















Nimeshawishika sana na kilimo cha maharage kama kaka **Mushi**. Swali langu ni hali gani ya hewa ambayo kilimo cha maharage ya njano kinakubali na ni muda gani maharage yanachukua tokea kupanda hadi kuvuna? Ahsante.
***SHABANI YUSUPH – Nyegezi, Mwanza***


Nataka nianze kilimo cha maharage mjini Mbeya, nimepata inspiration kubwa kutoka kwenu. Ahsante sana **Shujaaz**
***GEORGE LEORNARD - Tabata Kimanga, Dar-es- salaam***

Nataka kupanda maharage sasa. Ahsanteni, nimekua inspired sana na ***SHUJAAZ*** ila sikuelewa siku 28 inakuwaje, maharage yameshakomaa au? ***CHRISTINA – MOROGORO***


Mimi nina mpango wa kuanza kulima maharage, ahsante sana ***SHUJAAZ*** mmeni-inspire kinoma! ***NYAU ROSSO***

Nahitaji kuanza kulima maharage, mmenihimiza sana. Big up ***DJ Tee. CHIKU KHAMIS***

Majibu ya maswali haya yatapatikana kwenye ukurasa wa 26


KUNA WAKALI WALIOFURAHIA TU STORI ZA JESCA NA BWANA MUSHI... LAKINI KUNA WAKALI WALIOONA FURSA NDANI YAKE...
MMOJA WAO NI HAMISI WA MORO... YEYE ALISANULIWA VYA KUTOSHA SANA NA STORY YA JESCA NA MUSHI NA AKAAMUA KUCHANGAMKIA FURSA...
HAMISI – MOROGORO
"Kwa kweli story ya Maharage Bingwa ilinifanya niamke maana sikuwa na dili la kufanya…
Nilivutiwa sana na nikajaribu ukulima wa maharage ya soya mwaka jana. Nililima ekari 2 na mwezi wa 7 nilifanikiwa kuvuna magunia 25. Mavuno haya yalikua yenye mafanikio mno kwa sababu yameondoa shida nyingi nilizopata. Ahsante DJ Tee kwa stori zako zinazo-hamisha vijana"
SENGWA – ARUSHA
"Nimejihusisha kwenye kilimo cha maharage kwa muda mrefu sasa. Story ya Maharage Bingwa imeni-fungua macho zaidi na kwa mwaka huu nimefanikiwa kuvuna magunia zaidi ya kilo 120. Sasa hivi hii ndio kazi yangu. Maharage yananifanya niwe na uwezo wa kununua nikitakacho. Ahsante kwa kutusanua wana"
MWANA MWINGINE NI HUYU HAPA... NA YEYE HAKUSITA KUCHANGAMKIA FURSA!
NA BIDADA HAPA ALIJARIBU, NIMEVUTIWA SANA NA KUTO-KATA TAMAA KWAKE!
SHUJAAZ
Nilivutiwa sana niliposoma Maharage Bingwa, nikaanza kulima maharage ya njano, lakini nilishindwa kuyatunza vizuri kwa kukosa ujuzi wa kutosha. Nashukuru Shujaaz kwani sasa hivi nimepata nguvu mpya"
JENIFA - IPOGOLO, IRINGA
HAWA WANA NIMEWAKUBALI SANA KWA KUWA WALIAMUA KUCHANGAMKIA FURSA, KUJARIBU NA WAO KUWA MABINGWA WA MAHARAGE A.K.A MAHARAGE BINGWA!
SHUJAAZ





## CHANGAMOTO ZINAZOWAKUTA WAKULIMA WA MAHARAGE MARA KWA MARA

1. Majani ya maharage machanga kubadilika rangi na kukauka – Joto na ukosefu wa mvua.
2. Mavuno kidogo yasiyo na afya – Kutolima na kuhudumia maharage kitaalamu.
3. Mimea kufa baada ya kutumia mbolea – Ukosefu wa elimu kuhusu mbolea za kutumia na wakati muafaka wa kutumia.
4. Kutofahamu mbegu bora ni ipi – Ukosefu wa ujuzi kuhusu mbegu bora.
5. Mimea kuliwa na wadudu na magonjwa – Kutofahamu dawa zinazofaa na nini cha kufanya.






## 1. UANDAAJI WA ARDHI

* Hakikisha ardhi unayochagua haituamishi maji.
* Hakikisha ardhi haina kiasi kikubwa cha acid (Kibongobongo acid ni tindikali. Wataalamu wa udongo huwa wanapima hivi vitu).
* Safisha na lima matuta kuzuia mmomonyoko wa udongo.



USISAHAU KUOMBA USHAURI WA KITAALAMU KUTOKA KWA MTAALAMU WA KILIMO ALIYEPO KARIBU NAWE!

* Hakikisha udongo una unyevunyevu wakati unapanda mbegu za maharage.
* Panda mbegu kwenye mstari, hakikisha umbali kati ya mmea na mmea haupungui **sentimita 10**, na umbali wa tuta kwa tuta haupungui **sentimita 50**.

## 2. UCHAGUZI WA MBEGU BORA

* Jiulize ni muda gani unahitaji kuanzia kupanda hadi kuvuna. Je, unahitaji mbegu za muda mrefu au muda mfupi?



YAANI... UKIPANDA MIEZI YA MWISHO WA MWAKA AU KAMA ENEO ULIPO KUNA KIASI KIDOGO CHA MVUA BASI TUMIA MBEGU ZA MUDA MFUPI. ILA, MBEGU ZA MUDA MREFU ZINA FAIDA KWA KUWA HUTOA MAZAO KWA WINGI NA HURUTUBISHA ARDHI KUTOKANA NA NITROJENI.

* Jiulize ni aina ya maharage yanayostawi maeneo yenu. Je, ni ya kutambaa au ya kawaida? Fanya utafiti kabla hujaamua.
* Chagua mbegu zenye afya, zisizoharibika, kisha jaribisha uwezo wa mbegu ulizochagua. Chagua mbegu kadhaa (kama 50 hivi kisha uzipande kwanza). Kama ndani ya wiki moja 40 kati ya 50 zitachipua, basi mbegu zako ni bora.

SASA WEWE JITIE KICHWA NGUMU UKAPANDE MBEGU ZIMEOZA!





## 3. UTUMIAJI WA MBOLEA

* Maharage hujitengenezea naitrojeni yake yenyewe, kwa hiyo huna haja ya kutumia UREA au CAN.
* Tumia mbolea za **DAP, TSP, NPK, Sympal** au **Minjingu Phosphate** kwa ajili ya kuongeza madini ya phosphorous ambayo ni muhimu kwa ukuaji wa maharage.
* Weka mbolea kwenye mashimo utakayopanda maharage, kisha fukia mbolea kwa udongo kiasi, au unaweza kuchimba shimo jingine dogo pembeni ya mbegu kwa ajili ya mbolea.
* Unapoweka mbolea wakati wa kupanda, hakikisha udongo una unyevunyevu.

## 4. UPANDAJI



KWA TAARIFA YAKO UKIPANDA KWENYE MISTARI ITAKUSAIDIA KUPALILIA VIZURI NA KUVUNA BILA SHIDA!

* Kwa mbegu zinazotambaa, tumia fimbo au Kamba kuzitengenezea njia. Fimbo ndefu husaidia kuleta mazao mengi na njia hii ni nzuri kama huna ardhi kubwa.

## 5. UTUNZAJI WA SHAMBA

* Ondoa magugu kwa kupalilia angalau mara mbili kabla ya kuvuna. (Wiki ya pili baada ya kupanda, kisha wiki ya 5 au 6 baadae). Unaweza kuondoa magugu kwa jembe au dawa.

UKITAKA KUTOA MAGUGU KWA DAWA, CHEKI NA MTAALAMU WA KILIMO AKUPE MAELEKEZO YA KUTOSHA!



## 6. DAWA NA MAGONJWA

* Chunguza shamba lako mara kwa mara kuona kama kuna wadudu waharibifu
* Magonjwa maarufu ya maharage ni pamoja na bakapembe na kutu.
* Tumia mbegu sugu kwa magonjwa kuhakikisha magonjwa hayaathiri mazao yako.








## MASWALI YANAYOULIZWA SANA KUHUSU MAHARAGE...




NGOJA NIWAPE MAUJANJA WANA...
12:56 PM
54%
Aina gani ya udongo ni bora kwa ajili ya kilimo cha maharage?
Maharage huhitaji udongo usioshika maji na wenye rutuba. Pia, maharage hukua vizuri kwenye udongo wenye pH si chini ya 5.6
Ni aina gani bora ya maharage hustawi nchini Tanzania?
Kuna aina mbalimbali za maharage zinazostawi katika maeneo mbalimbali. Njano Uyole, Uyole 04, Lyamungu 90 na Jesca ni kati ya mbegu zenye mavuno mazuri na sugu kwa baadhi ya magonjwa ya maharage. Unapoenda kununua mbegu, ulizia aina bora kwa eneo ulilopo.
Ni mbolea gani zinapaswa kutumika ili maharage yakue vizuri?
Kikawaida, maharage hujitengenezea naitrojeni yake yenyewe, hivyo hakuna haja ya kutumia mbolea kama UREA au CAN lakini kwa ajili ya virutubisho vingine, tumia mbolea zenye phosphorus wakati wa kupanda, kama: TSP, DAP, Minjingu na NPK.
Ni mikoa gani ya Tanzania ni bora kwa ajili ya kilimo cha maharage?
Mikoa ya Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini ni bora. Mfano: Arusha, Kilimanjaro na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Tanga hasa Lushoto na Korogwe; pia Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe na Mbeya.
SMS
JE, UMESHAWAHI KUFANYA KILIMO CHA MAHARAGE NA NINI AMBACHO UNGEPENDA UKIFAHAMU KUHUSU KILIMO HIKI? NITUMIE SMS KWENDA 0784551616 UKIANZA NA NENO #BEANS
TUMA SMS KALI UPATE CHANCE YA KUJISHINDIA ZAWADI KALI!